13

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
ZANZIBAR

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR,

# MWAKA, 2023

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWAKA, 2023

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukusanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).


## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA


Jumla ya matukio 1,954 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwaka, 2023 ambapo waathirika walikuwa 1,959. Waathirika wengi walikuwa watoto sawa na asilimia 83.7, wanawake asilimia 12.0 na wanaume asilimia 4.3. Miongoni mwa watoto waathirika; wasichana walikuwa 1,263 (asilimia 77.1) na wavulana walikuwa 376 (asilimia 22.9).

**Kielelezo 1.1: Asilimia ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwaka 2023**




Idadi ya Matukio ya Kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 925, ambapo waathirika 826 walikuwa wasichana na 99 walikuwa wanawake. Matukio ya kulawiti yalikuwa 247 ambapo waathirika 237 walikuwa wavulana na 10 walikuwa wanaume. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile ni 90 ambapo wasichana walikuwa 79 na 11 walikuwa wanawake. Matukio ya kutorosha ni 110 ambapo waathirika sita (6) walikuwa wanawake , waathirika 102 walikuwa wasichana na wawili walikuwa wavulana . Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu ni 211 ambapo waathirika 46 ni wanawake,145 walikuwa wasichana , waathirika 18 walikuwa wavulana na waathirika wawili (2) ni wanaume. Matukio ya shambulio yalikuwa 376 ambapo waathirika 111 walikuwa wasichana, 119 walikuwa wavulana, 74 walikuwa wanawake na 72 walikuwa wanaume.

**Kielelezo 1.2 Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa KijinsiaMwaka, 2023**




Wilaya ya Mjini imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 457) sawa na asilimia 23.4 ikifuatia wilaya ya Magharibi "A" ambapo yameripotiwa matukio 433 (asilimia 22.2). Wilaya ya Micheweni imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, matukio 42 sawa na asilimia 2.1 ukilinganisha na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mwaka, 2023**




Idadi ya matukio yameongezeka kwa asilimia 43.7 kufikia matukio 1,954 mwaka, 2023 kutoka matukio 1,360 mwaka, 2022. Matukio yote yameripotiwa kuongezeka kwa mwaka 2023.

Wilaya ya Mjini imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 457) kwa mwaka, 2023 ambapo wilaya ya Magharibi "B" iliripotiwa kuongoza zaidi kwa mwaka, 2022 (matukio 288).

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mwaka, 2022 na Mwaka, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyumena Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Mwaka 2022 | Mwka 2023 | Mwaka 2022 | Mwka 2023 | Mwaka 2022 | Mwka 2023 | Mwaka 2022 | Mwka 2023 | Mwaka 2022 | Mwka 2023 | Mwaka 2022 | Mwka 2023 | Mwaka 2022 | Mwka 2023 |
| Kaskazini 'A' | 52 | 98 | 32 | 59 | 8 | 11 | 4 | 4 | 4 | 8 | 4 | 10 | 0 | 6 |
| Kaskazini 'B' | 59 | 113 | 39 | 74 | 8 | 15 | 1 | 0 | 0 | 1 | 6 | 15 | 5 | 8 |
| Kati | 110 | 94 | 62 | 51 | 19 | 13 | 16 | 16 | 7 | 3 | 6 | 11 | 0 | 0 |
| Kusini | 47 | 45 | 30 | 25 | 3 | 4 | 2 | 3 | 7 | 2 | 5 | 11 | 0 | 0 |
| Mjini | 279 | 457 | 116 | 179 | 47 | 63 | 26 | 9 | 4 | 19 | 18 | 30 | 68 | 157 |
| Magharibi 'A' | 253 | 433 | 106 | 190 | 40 | 42 | 17 | 25 | 10 | 20 | 30 | 45 | 50 | 111 |
| Magharibi 'B' | 288 | 417 | 130 | 188 | 45 | 61 | 17 | 28 | 14 | 20 | 23 | 27 | 59 | 93 |
| Wete | 115 | 93 | 48 | 38 | 12 | 20 | 3 | 4 | 17 | 11 | 9 | 20 | 26 | 0 |
| Micheweni | 39 | 42 | 25 | 32 | 1 | 4 | 1 | 1 | 2 | 3 | 6 | 2 | 4 | 0 |
| Chake Chake | 76 | 108 | 36 | 57 | 11 | 13 | 1 | 0 | 15 | 12 | 13 | 26 | 0 | 0 |
| Mkoani | 42 | 54 | 27 | 30 | 6 | 0 | 0 | 0 | 4 | 10 | 5 | 13 | 0 | 1 |
| **Zanzibar** | **1,360** | **1,954** | **651** | **923** | **200** | **246** | **88** | **90** | **84** | **109** | **125** | **210** | **212** | **376** |

Miongoni mwa watoto 1,639 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 826, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 237, Kuingilia kinyume na maumbile ni wasichana 79, Kutorosha ni 104 ambapo wasichana walikuwa 102 na wavulana walikuwa wawili (2), shambulio la aibu ni 163 kati yao wasichana walikuwa 145 na wavulana 18 na shambulio walikuwa 230 kati yao wasichana walikuwa 111 na wavulana walikuwa 119.

**Jadweli 1.2: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya Mwaka, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 77 | 49 | 11 | 3 | 8 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 93 | 66 | 15 | 0 | 1 | 0 | 9 | 0 | 2 | 0 |
| Kati | 82 | 43 | 13 | 16 | 3 | 0 | 5 | 2 | 0 | 0 |
| Kusini | 37 | 20 | 4 | 2 | 2 | 0 | 6 | 3 | 0 | 0 |
| Mjini | 362 | 155 | 60 | 8 | 17 | 0 | 24 | 0 | 48 | 50 |
| Magharibi 'A' | 352 | 169 | 38 | 21 | 18 | 1 | 35 | 2 | 33 | 35 |
| Magharibi 'B' | 361 | 172 | 59 | 26 | 19 | 0 | 23 | 0 | 28 | 34 |
| Wete | 87 | 36 | 19 | 3 | 11 | 0 | 13 | 5 | 0 | 0 |
| Micheweni | 41 | 32 | 4 | 0 | 3 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 100 | 55 | 14 | 0 | 10 | 1 | 16 | 4 | 0 | 0 |
| Mkoani | 47 | 29 | 0 | 0 | 10 | 0 | 7 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **1,639** | **826** | **237** | **79** | **102** | **2** | **145** | **18** | **111** | **119** |

Miongoni mwa wanawake 236 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa 99, kuingilia kinyume na maumbile ni 11, kutorosha ni sita (6), shambulio la aibu walikuwa wanawake 46 na shambulio walikuwa wanawake 74.

**Jadweli 1.3a: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Mwaka, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia Kinyumena Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 21 | 10 | 1 | 0 | 4 | 6 |
| Kaskazini 'B' | 19 | 8 | 0 | 0 | 5 | 6 |
| Kati | 12 | 8 | 0 | 0 | 4 | 0 |
| Kusini | 8 | 5 | 1 | 0 | 2 | 0 |
| Mjini | 60 | 24 | 1 | 2 | 6 | 27 |
| Magharibi 'A' | 53 | 21 | 4 | 1 | 7 | 20 |
| Magharibi 'B' | 37 | 16 | 2 | 1 | 4 | 14 |
| Wete | 5 | 2 | 1 | 0 | 2 | 0 |
| Micheweni | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 13 | 4 | 0 | 2 | 7 | 0 |
| Mkoani | 7 | 1 | 0 | 0 | 5 | 1 |
| **Zanzibar** | **236** | **99** | **11** | **6** | **46** | **74** |

Miongoni mwa wanaume 84 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanaume waliolawitiwa walikuwa 10, Shambulio la Kukashifu / shambulio la aibu ni wawili (2) na shambulio walikuwa wanaume 72.

**Jadweli 1.3b: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Mwaka, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Aibu/ Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 35 | 3 | 0 | 0 | 32 |
| Magharibi 'A' | 28 | 4 | 0 | 1 | 23 |
| Magharibi 'B' | 19 | 2 | 0 | 0 | 17 |
| Wete | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **84** | **10** | **0** | **2** | **72** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 822) sawa na asilimia 50.2 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 433) sawa na asilimia 26.4. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 538) sawa na asilimia 65.1 ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.4: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri Mwaka, 2023**

| Miaka | Aina ya Ukatili naUdhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 35 | 26 | | | 6 | 0 | 0 | 8 | 29 | 0 | 0 | 104 |
| 6-10 | | 64 | 105 | | | 23 | 0 | 1 | 5 | 46 | 20 | 16 | 280 |
| 11-14 | | 189 | 72 | | | 25 | 1 | 21 | 2 | 30 | 42 | 51 | 433 |
| 15-17 | | 538 | 34 | | | 25 | 1 | 80 | 3 | 40 | 57 | 44 | 822 |
| **Jumla** | | **826** | **237** | | | **79** | **2** | **102** | **18** | **145** | **119** | **111** | **1,639** |

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwaka, 2023 yameongezeka kwa asilimia 39.7 kufikia matukio 1,639 kwa mwaka 2023 kutoka 1,173 kwa mwaka 2022. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa makundi yote yameongezeka kwa mwaka 2023.

**Jadweli 1.5: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri, Mwezi Mwaka 2022 na Mwaka 2023**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Mwaka 2022 | Jumla Mwaka 2023 |
| | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 | | |
| 0-5 | 16 | 35 | 18 | 26 | 4 | 6 | 5 | 0 | 18 | 37 | 0 | 0 | 61 | 104 |
| 6-10 | 52 | 64 | 86 | 105 | 33 | 23 | 2 | 1 | 40 | 51 | 16 | 36 | 229 | 280 |
| 11-14 | 164 | 189 | 75 | 72 | 27 | 25 | 17 | 22 | 21 | 32 | 43 | 93 | 347 | 433 |
| 15-17 | 353 | 538 | 18 | 34 | 20 | 25 | 55 | 81 | 12 | 43 | 78 | 101 | 536 | 822 |
| **Jumla** | **585** | **826** | **197** | **237** | **84** | **79** | **79** | **104** | **91** | **163** | **137** | **230** | **1,173** | **1,639** |


Watu wenye umri wa miaka 18-29 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 282) sawa na asilimia 88.1 ya matukio yote ya wanawake na wanaume yalioripotiwa ikifuatiwa na watu wenye umri wa miaka 30-39 (matukio 28) sawa na asilimia 8.8. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 18-29 (matukio 85) sawa na asilimia 85.9 ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.5a: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume na Wanawake kwa Umri Mwaka, 2023**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | |
| | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake | |
| 18-29 | | 85 | 9 | | | 10 | 0 | 6 | 1 | 38 | 69 | 64 | 282 |
| 30-39 | | 8 | 0 | | | 1 | 0 | 0 | 1 | 6 | 3 | 9 | 28 |
| 40-49 | | 3 | 1 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 5 |
| 50-59 | | 2 | 0 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 4 |
| 60-69 | | 1 | 0 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 70-79 | | 0 | 0 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 80+ | | 0 | 0 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | | **99** | **10** | | | **11** | **0** | **6** | **2** | **46** | **72** | **74** | **320** |

Matukio mengi zaidi (matukio 660) yametokea Nyumbani kwa Mtuhumiwa sawa na asilimia 33.7 ikifuatiwa na matukio yaliyotokea Sehemu nyengine(matukio 626) sawa na asilimia 32.0 ukilinganisha na maeneo mengine yaliyotajwa.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Mwaka, 2023**




Matukio 629 kati ya matukio 1,954 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 32.2, matukio 81 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 4.1, matukio 838 yamepelekwa mahakamani sawa na asilimia 42.9 , matukio 29 yameondolewa Mahakamani sawa na asilimia 1.5, matukio matatu (3) yamefungwa na Polisi sawa na asilimia 0.2 na matukio 374 yametiwa hatiani sawa na asilimia 19.1.

**Jadweli 1.6: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Mwaka, 2023**

| Aina ya Matukio | Aina ya Matukio | Watu wazima | | Watoto | | Zinazoendelea Mahakamani | Zilizopata hatia | Zilizochini ya Upelelezi | Zilizopelekwa kwa DPP | Zilizoondolewa Mahakamani | Zilizofungwa Polisi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Wanaume | Wasichana | Wavulana | | | | | | |
| Kubaka | 923 | 99 | | 826 | | 378 | 204 | 252 | 60 | 26 | 3 |
| Kulawiti | 246 | | 10 | | 237 | 101 | 53 | 82 | 9 | 1 | 0 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 90 | 11 | | 79 | | 42 | 16 | 30 | 2 | 0 | 0 |
| Kutorosha | 109 | 6 | 0 | 102 | 2 | 39 | 20 | 49 | 0 | 1 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 210 | 46 | 2 | 145 | 18 | 96 | 37 | 70 | 7 | 0 | 0 |
| Shmabulio | 376 | 74 | 72 | 111 | 119 | 182 | 44 | 146 | 3 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **1,954** | **236** | **84** | **1,263** | **376** | **838** | **374** | **629** | **81** | **29** | **3** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa kwa mwaka 2023 walikuwa 1,970 kati yao, 1,518 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 77.1 na 427 walikuwa jirani sawa na asilimia 21.7.

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Mwaka, 2023**



## TAKWIMU ZA UDHALILISHAJI KWA WATU WENYE ULEMAVU, MWAKA 2023

Jumla ya watu 13 wenye ulemavu wamefanyiwa ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa mwaka 2023. Ambapo wanawake walikuwa sita (6), wanaume wawili (2),wasichana wanne (4) na mvulana mmoja (1).

Wilaya ya Chakechake imeripotiwa kuwa na watu wengi zaidi wenye ulemavu (wanne(4)).

**Jadweli 2.1: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji kwa Watu wenye Ulemavu kwa Wilaya na Jinsi, Mwaka 2023**

| Wilaya | Wanawake | Wanaume | Wasichana | Wavulana | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini "A" | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 |
| Kaskazini "B" | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi "A" | 1 | 0 | 1 | 0 | 2 |
| Magharibi "B" | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Chakechake | 2 | 0 | 2 | 0 | 4 |
| Mkoani | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **6** | **2** | **4** | **1** | **13** |

Waathirika wa ubakaji wanane(8) kati ya waathirika 13 wa watu wenye ulemavu waliofanyiwa udhalilishaji, , waathirika waliolawitiwa walikuwa watatu(3), kuingilia kinyume na maumbile ni mmoja (1) na kukashifu mmoja(1).

**Jadweli 2.2: Aina ya Matukio ya Udhalilishaji kwa Watu wenye Ulemavu kwa Jinsi, Mwaka 2023**


| Jinsi | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na Maumbile | Kukashifu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Wanawake | 5 | [redacted] | 1 | 0 | 6 |
| Wanaume | [redacted] | 2 | [redacted] | 0 | 2 |
| Wasichana | 3 | [redacted] | 0 | 1 | 4 |
| Wavulana | [redacted] | 1 | [redacted] | 0 | 1 |
| **Jumla** | **8** | **3** | **1** | **1** | **13** |

## WANAFUNZI NA MAHABUSU WA MAKOSA YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA WA CHUO CHA MAFUNZO

Jumla ya Wanafunzi wa makosa ya ukatili na udalilishaji wa kijinsia  waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa mwaka, 2023 walikuwa 111 na Mahabusu walikuwa 344.


Kati ya Wanafunzi waliopokelewa wengi wao walitokea Wilaya ya Mjini ambao ni 45 ukilinganisha na wilaya nyengine.  Idadi kubwa ya mahabusu wamepokelewa kutokea Wilaya ya Mjini (mahabusu 138).

**Kielelezo 4.1: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Wilaya, Mwaka, 2023**




Umri wa miaka 18-29 umeripotiwa kuwa na wanafunzi na mahabusu wengi zaidi  ikilinganishwa na miaka mengine, ambapo Wanafunzi walikuwa 69 na Mahabusu ni 166.

**Kielelezo 4.2: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Umri, Mwaka, 2023**



Kati ya Wanafunzi 111 waliopokelewa Chuo cha Mafunzo, wengi wao wamehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 11 na zaidi (wanafunzi 70) sawa na asilimia 63.1 ikilinganishwa na muda mwengine wa kutumikia vifungo.

**Jadweli 4.3: Idadi ya Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kwa Muda wa Vifungo na Aina ya Makosa, Mwaka, 2023**

| Muda wa kutumikia kifungo Chuoni (Gerezani) | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | |
| Chini ya miezi 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 6 |
| Miezi 4-11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 2 | 6 |
| Mwaka 1-2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 4 | 11 |
| Miaka 3-5 | 0 | 0 | 0 | 3 | 3 | 0 | 6 |
| Miaka 6-10 | 0 | 2 | 3 | 3 | 4 | 0 | 12 |
| Miaka 11+ | 32 | 15 | 9 | 14 | 0 | 0 | 70 |
| **Jumla** | **32** | **17** | **12** | **20** | **24** | **6** | **111** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6). Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 1,954 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwaka, 2023 ambapo waathirika walikuwa 1,959. Wilaya ya Mjini imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 457) sawa na asilimia 23.4. Idadi ya matukio kwa yameongezeka kwa asilimia 43.7 kufikia matukio 1,954 mwaka, 2023 kutoka matukio 1,360 kwa mwaka, 2022.

Matukio 629 kati ya matukio 1,954 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 32.2, matukio 81 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 4.1,matukio 838 yamepelekwa mahakamani sawa na asilimia 42.9 , matukio 29 yameondolewa Mahakamani sawa na asilimia 1.5, matukio matatu (3) yamefungwa na Polisi sawa na asilimia 0.2 na matukio 374 yametiwa hatiani sawa na asilimia 19.1.

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Mwaka, 2023**

| Eneo la Matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani kwa Muathirika | 72 | [redacted] | 72 | [redacted] | 9 | 9 | 5 | [redacted] | 5 | 6 | 0 | 6 | 54 | 2 | 56 | 65 | 53 | 119 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 330 | [redacted] | 330 | [redacted] | 80 | 80 | 48 | [redacted] | 48 | 55 | 1 | 56 | 48 | 4 | 52 | 50 | 44 | 94 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 86 | [redacted] | 86 | [redacted] | 10 | 10 | 3 | [redacted] | 3 | 10 | 0 | 10 | 6 | 0 | 6 | 9 | 10 | 19 |
| Sehemu za kazi | 3 | [redacted] | 3 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 9 | 10 | 19 |
| Skuli/ Madrasa | 2 | [redacted] | 2 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 152 | [redacted] | 152 | [redacted] | 50 | 50 | 15 | [redacted] | 15 | 8 | 0 | 8 | 13 | 1 | 14 | 1 | 3 | 4 |
| Sehemu nyengine(Vichakanina kwengine) | 280 | [redacted] | 280 | [redacted] | 98 | 98 | 19 | [redacted] | 19 | 28 | 1 | 29 | 66 | 13 | 79 | 51 | 71 | 121 |
| **Jumla** | **925** | [redacted] | **925** | [redacted] | **247** | **247** | **90** | [redacted] | **90** | **107** | **2** | **109** | **191** | **20** | **211** | **185** | **191** | **376** |

**Jadweli 2.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mwaka, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 98 | 59 | 11 | 4 | 8 | 10 | 6 |
| Kaskazini 'B' | 113 | 74 | 15 | 0 | 1 | 15 | 8 |
| Kati | 94 | 51 | 13 | 16 | 3 | 11 | 0 |
| Kusini | 45 | 25 | 4 | 3 | 2 | 11 | 0 |
| Mjini | 457 | 179 | 63 | 9 | 19 | 30 | 157 |
| Magharibi 'A' | 433 | 190 | 42 | 25 | 20 | 45 | 111 |
| Magharibi 'B' | 417 | 188 | 61 | 28 | 20 | 27 | 93 |
| Wete | 93 | 38 | 20 | 4 | 11 | 20 | 0 |
| Micheweni | 42 | 32 | 4 | 1 | 3 | 2 | 0 |
| Chake Chake | 108 | 57 | 13 | 0 | 12 | 26 | 0 |
| Mkoani | 54 | 30 | 0 | 0 | 10 | 13 | 1 |
| **Zanzibar** | **1,954** | **923** | **246** | **90** | **109** | **210** | **376** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Mwaka, 2022 na Mwaka, 2023**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 |
| Kubaka | 651 | 923 | 66 | 99 | 585 | 826 | | | | |
| Kulawiti | 200 | 246 | | | | | 197 | 237 | 3 | 10 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 88 | 90 | 5 | 11 | 84 | 79 | | | | |
| Kutorosha | 84 | 109 | 5 | 6 | 78 | 102 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 125 | 210 | 34 | 46 | 79 | 145 | 12 | 18 | 0 | 2 |
| Shambulio | 212 | 376 | 75 | 74 | 63 | 111 | 74 | 119 | 0 | 72 |
| **Jumla** | **1,360** | **1,954** | **185** | **236** | **889** | **1,263** | **284** | **376** | **3** | **84** |

**Kielelezo 4.1: Idadi ya Wanafunzi Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Wilaya na Aina ya Matukio, Mwaka, 2023**

| Wilaya | Idadi ya wanafunzi | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 5 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 6 | 2 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 45 | 12 | 9 | 5 | 8 | 8 | 3 |
| Magharibi 'A' | 17 | 3 | 3 | 4 | 2 | 4 | 1 |
| Magharibi 'B' | 20 | 5 | 1 | 1 | 5 | 6 | 2 |
| Wete | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 10 | 4 | 2 | 1 | 0 | 3 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **111** | **32** | **17** | **12** | **20** | **24** | **6** |

**Kielelezo 4.2: Idadi ya Wanafunzi Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwaka, 2023**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | |
| 15-17 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 |
| 18-29 | 17 | 12 | 9 | 11 | 16 | 4 | 69 |
| 30-39 | 9 | 4 | 2 | 6 | 4 | 2 | 27 |
| 40-49 | 4 | 1 | 1 | 2 | 3 | 0 | 11 |
| 50-59 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 |
| 60-69 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70-79 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 80+ | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **32** | **17** | **12** | **20** | **24** | **6** | **111** |

**Kielelezo 4.3: Idadi ya Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Wilaya na Aina ya Matukio, Mwaka, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Mahabusu | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | Kumuingilia kimwili magharimu wake |
| Kaskazini 'A' | 6 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 14 | 2 | 3 | 2 | 4 | 3 | 0 | 0 |
| Kati | 22 | 4 | 6 | 3 | 2 | 4 | 3 | 0 |
| Kusini | 8 | 2 | 2 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 |
| Mjini | 138 | 34 | 27 | 14 | 25 | 21 | 17 | 0 |
| Magharibi 'A' | 58 | 14 | 9 | 5 | 11 | 12 | 7 | 0 |
| Magharibi 'B' | 78 | 18 | 16 | 12 | 15 | 9 | 8 | 0 |
| Wete | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 17 | 3 | 0 | 2 | 4 | 5 | 3 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **344** | **80** | **63** | **39** | **63** | **57** | **42** | **0** |

**Kielelezo 4.4: Idadi ya Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwaka, 2023**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | Kumuingilia kimwili magharimu wake | Jumla |
| 15-17 | **5** | **0** | **0** | **8** | **0** | **0** | **0** | **13** |
| 18-29 | 38 | 27 | 18 | 32 | 28 | 23 | 0 | 166 |
| 30-39 | 26 | 19 | 12 | 17 | 21 | 17 | 0 | 112 |
| 40-49 | 9 | 11 | 7 | 5 | 8 | 2 | 0 | 42 |
| 50-59 | 2 | 6 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 11 |
| 60-69 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70-79 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 80+ | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **80** | **63** | **39** | **63** | **57** | **42** | **0** | **344** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:**

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136
MMP, Zanzibar.